

TAARIFA YA MATOKEO YA MITIHANI YA KIDATO CHA PILI, DARASA LA SITA NA DARASA LA NNE MWAKA 2016

Ndugu Wazazi, Wanafunzi, Walimu na Wananchi wote kwa ujumla itakumbukwa kwamba Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Pili, darasa la Sita na darasa la Nne ilifanyika tarehe 16/11/2016 hadi tarehe 06/12/2016.

Mitihani yote hii ilishirikisha skuli zote za serikali na za binafsi. Kwa mwaka 2016 kwa mara ya kwanza umefanyika mtihani wa darasa la nne wenye lengo la kupima na kutathmini kiwango cha elimu ya msingi (chini).

MTIHANI WA KIDATO CHA PILI

- Jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni **27,017** wakiwemo wanawake **14,195** sawa na asilimia **52.5** na wanaume **12,822** sawa na asilimia **47.5**. Hili ni ongezeko la asilimia **6.7** ukilinganisha na mwaka 2015.
- Wanafunzi waliofanya mtihani ni **25,087** sawa na asilimia **92.9** ya walioandikishwa wakiwemo wanawake **13,414** sawa na asilimia **53.5** na wanaume **11,673** sawa na asilimia **46.5**.
- Wanafunzi **17,581** sawa na asilimia **70.1** wamefaulu na kuchaguliwa kuingia Kidato cha Tatu 2017 wakiwemo wanawake **10,084** sawa na asilimia **57.4** na wanaume **7,497** sawa na asilimia **42.6**. Hili ni ongezeko la asilimia **0.5** ukilinganisha na mwaka uliopita wa 2015.

MTIHANI WA DARASA LA SITA

- Jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni **33,250** wakiwemo wanawake **17,183** sawa na asilimia **51.9** na wanaume **16,067** sawa na asilimia **48.1**. Hili ni ongezeko la asilimia **21.4** ukilinganisha na mwaka uliopita wa 2015.
- Wanafunzi waliofanya mtihani ni **30,889** sawa na asilimia **92.9** ya walioandikishwa wakiwemo wanawake **16,413** sawa na asilimia **53.1** na wanaume **14,476** sawa na asilimia **46.9**.
- Jumla ya wanafunzi **2,361** sawa na asilimia **7.1** ya wanafunzi walioandikishwa mtihani huu hawakufanya mitihani.
- Wanafunzi **29,413** sawa na asilimia **95.2** wamefaulu na kuchaguliwa kuingia Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2017 wakiwemo wanawake **16,087** sawa na asilimia **52.0** na wanaume **13,326** sawa na asilimia **48.0**. Huu ni upungufu wa asilimia **4.4** ukilinganisha na mwaka uliopita wa 2015.
- Jumla ya wanafunzi **71** wamechaguliwa kujiunga na madarasa ya vipawa na wanafunzi **889** wamechaguliwa kujiunga na madarasa ya michepuo.

MTIHANI WA DARASA LA NNE

- Jumla ya wanafunzi walioandikishwa ni **38,696** wakiwemo wanawake **19,435** sawa na asilimia **50.2** na wanaume **19,261** sawa na asilimia **49.8**.
- Wanafunzi waliofanya mtihani ni **34,681** sawa na asilimia **89.2** ya walioandikishwa, wakiwemo wanawake **18,211** sawa na asilimia **52.5** na wanaume **14,470** sawa na asilimia **47.5**.

- Jumla ya wanafunzi **4,015** sawa na asilimia **10.4** ya waliandikishwa hawakufanya mtihani huu.
- Lengo kuu la kufanya mtihani huu wa darasa la nne kwa masomo manne tu ilikuwa ni kupima na kutathmini kiwango cha elimu kwa madarasa ya msingi (chini) ili kuimarisha ufundishaji katika madarasa hayo.

WANAFUNZI BORA KWA JUMLA KWA DARASA LA NNE

NO	JINA	SKULI
1.	Sara Juma said	Maahad Istiqama
2.	Shahar Saleh Kassim	Mwanakwerekwe 'F'
3.	Salhia Amir Said	Mitiulaya

WANAFUNZI BORA KWA JUMLA KWA DARASA LA SITA

NO	JINA	SKULI
1.	Said Ali Hamad	Kilimahewa 'A'
2.	Othman Ali Moh'd	Kidoti
3.	Said Badal Amour	Mwanakwerekwe 'E'

WANAFUNZI BORA KIDATO CHA PILI

NO	JINA	SKULI
1.	Ali Juma Said	Lumumba
2.	Aisha Said Ali	Chasasa
3.	Raya Nassor Ahmed	Fidel Castro

SKULI ZENYE WASTANI MKUBWA KITAIFA

NO	DARASA LA NNE	DARASA LA SITA	KIDATO CHA PILI
1.	GLORIOUS	ALI KHAMIS CAMP	FIDEL CASTRO
2.	ALI KHAMIS CAMP	GLORIOUS	LUMUMBA
3.	LAUREATE	FEZA	MADUNGU 'B'

SKULI ZENYE WASTANI MDOGO KITAIFA

NO	DARASA LA NNE	DARASA LA SITA	KIDATO CHA PILI
1.	MBUYUTENDE	KIBENI	MATEMWE
2.	CHAMBANI	KANDWI	KIZIMKAZI
3.	KANDWI	CHAMBANI	MAKONGENI

KESI ZA UDANGANYIFU

Kwa mwaka 2016 jumla ya watahiniwa tisa (9) wa Kidato cha Pili walithibitika kufanya udanganyifu. Wanafunzi wote hao wamefutiwa matokeo yao.

Kwa niaba ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, tunawapongeza wale wote waliofanikiwa kuendelea na masomo na tunawatakia kila la kheri katika changamoto zinazowakabili za masomo ya juu.

Aidha, tunawajuilisha wazazi na walimu wakuu kwamba wanafunzi wote wa madarasa ya Nne na Sita ambao hawakufanya mitihani husika kwa sababu zozote zile watalazimika kurudia madarasa hayo na kufanya tena mitihani mwisho wa mwaka 2017.

Kwa wanafunzi wa Kidato cha Pili ambao hawakufaulu tunawasihi wasivunjike moyo na tunawashauri Wazazi/Walezi wawapeleke kwenye Vituo vya Kujiendeleza viliopo karibu nao.

Wanafunzi waliofaulu kipawa na michepuo tu ndio watatangaziwa kwenye ZBC – Redio. Wanafunzi wa Kidato cha Pili matokeo yao yatapatikana katika skuli zao walizofanyia mitihani au kupitia tovuti ya Wizara ambayo ni www.moez.go.tz .

MWISHO

Wizara inatoa shukrani za dhati kwa Wazazi, Walimu, Vikosi vya SMZ, Wizara ya Mawasiliano, Wizara ya Habari na Utamaduni, Wizara ya Afya na wale wote walioshirikiana nasi katika kufanikisha kazi hii muhimu sana ya Mitihani ya Taifa.

Ahsanteni.